Nuru ya Kiswahili, Juzuu 3(1), Juni 2024: 43-69
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru31.4369

# Riwaya ya *Rosa Mistika*: Kurunzi ya Malezi ya Vijalunga

**Athumani S. Ponera**
**Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Dodoma**
athuman.ponera@udom.ac.tz

**Ikisiri**
Lengo la makala hii ni kujadili namna riwaya ya Kiswahili inavyosawiri suala la malezi katika familia, hususani malezi ya vijalunga. Makala inaangazia zila za changamoto za vijalunga pamoja na changamoto zenyewe; hatimaye, inapendekeza mikakati ya kuzidhibiti zila hizo. Utafiti na mjadala vimefanywa kwa kutumia Nadharia ya Uhalisia. Data zilikusanywa kwa kutumia njia za uchambuzi wa matini. Matokeo yanaonesha kuwa, kwa jumla, kiini cha matatizo ya vijalunga ni upogo wa malezi wanayoyapata katika familia au asasi za kielimu. Hali hii inasababisha vijalunga kunasa katika zila zinazowazunguka katika maisha yao. Matokeo hayo yamebainisha zila zifuatazo: mabadiliko ya mahitaji ya vijalunga, wazazi au walezi kukosa elimu ya kuishi na vijalunga, pamoja na kupwaya kwa mikakati ya umma kuhusu maisha ya vijalunga. Makala imebainisha kuwa zila hizo zinazaa changamoto zifuatazo: kukosa haki ya malezi, vijalunga kupata ujauzito wakiwa masomoni, kuambukizwa magonjwa, na kutengwa. Kutokana na zila na changamoto zilizobainishwa, mambo yafuatayo yanapendekezwa ili kujenga ustawi wa vijalunga. Mosi, wazazi na walezi wapatiwe elimu ya kuishi na vijalunga. Pili, utoaji wa elimu kuhusu mabadiliko ya mahitaji ya vijalunga uimarishwe. Tatu, mikakati ya umma kuhusu maisha ya vijalunga iimarishwe. Hatimaye, kupitia hoja hizo, tumedhihirisha kuwa riwaya ya *Rosa Mistika* inafaa kuwa kurunzi ya malezi ya vijalunga ikiwa itasomwa au kufundishwa kwa umakini.

**Dhana za msingi**: malezi, vijalunga, zila

## Utangulizi

Kijalunga ni mtu aliye katika rika la ujalunga, yaani umri wa kati ya utoto na utu uzima (Arnnet, 1999). Mulokozi (2017) anaweka bayana zaidi kuwa kijalunga ni mtu mwenye umri wa kubalehe, yaani miaka 12 hadi 21. McNeely (2003) anaeleza pia kuwa ujalunga ni hatua ya pili ya maisha ya mwanadamu ambayo huambatana na mabadiliko makubwa ya kimwili na kiakili. Kutokea kwa mabadiliko hayo huufanya umri huu kuwa kipindi hatari katika makuzi ya mwanadamu. Hatari hiyo huweza kutokea katika vipengele kama vile utangamano wa kijalunga na wanajamii wenzake au kufanya matendo au uamuzi unaoweza kuathiri maisha yake yajayo.

Kwa mujibu wa wataalamu kama vile Bakize (2004) na Shima (2021), uelezeaji na uainishaji wa marika mbalimbali ya watu (kama vile utoto, ujalunga, ujana, utu-uzima, na uzee) si jambo rahisi. Hali hii hutokana na ukweli kuwa uanishaji huo hufanywa kwa kuzingatia miktadha na vigezo vinavyotofautiana. Kwa hiyo, umri wa ujalunga hutofautiana kutokana na vigezo kama vile mahali, utamaduni, sheria, na matakwa ya mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa (Kaplan, 2004; Degner, 2007). Kwa mujibu wa Arnnet (1999) na Berlin (2009), zifuatazo ni sifa bainifu za umri wa ujalunga: Mosi, kijalunga hutokewa na mabadiliko katika mwili (kibayolojia, kiakili, na kimaono). Pili, hupata hamu ya kuwa huru na kujitegemea. Tatu, hupata ari ya kujenga utambulisho wake maalumu. Nne, hujawa na matarajio makubwa kuhusu maisha yake ya baadaye. Tano, huwa katika mtanziko wa kiutambuzi (kutokana na kuwa katika kipindi cha mpito cha mhamo kutoka utoto kwenda ujanani). Sita, hupenda kujiambatisha na vikundi vya vijalunga wenzake. Saba, hujifunza kwa urahisi sana tabia

mpya (nzuri au mbaya). Nane, huchagua na kutambulisha machaguo na/au mapendeleo yanayompa ridhiko la nafsi.

Sehemu kubwa ya sifa za ujalunga zilizobainishwa katika aya iliyotangulia husababisha kuwapo kwa hali ya kupishana au kusuguana baina ya vijalunga na wazazi au walezi. Vijalunga huhusishwa, kwa kiasi kikubwa, na tabia hasi kama vile ulevi, matumizi ya dawa za kulevya, na kujinyonga. Hali hiyo ya vijalunga kuhusishwa na tabia hasi huchagizwa na zila. Tunatumia neno zila kama kisawe cha neno la Kiingereza *zeal*, yaani ghera, kani, msukumo au ari ya kufanya jambo (TUKI, 2006). Kwa muktadha wa kifasihi, zila humaanisha kosa la kimatendo, kimaneno au kiuamuzi ambalo huwa chanzo cha matokeo au hali hasi (Wamitila, 2003). Mifano ya matokeo au hali hasi ni anguko la hadhi au kupatwa na jambo lolote linaloweza kusababisha utanzia (kama vile maradhi, sononeko, au msawajiko).

Kwa kuwa fasihi huakisi mambo yanayotokea katika jamii (Senkoro, 2011; TET, 2019), kuwako kwa watu wa rika la ujalunga katika jamii pamoja na matatizo mbalimbali yanayowatokea vijalunga husawiriwa pia katika kazi mbalimbali za fasihi, zikiwamo riwaya. Kundi la vijalunga hutumiwa katika riwaya mbalimbali kama wahusika, kama ilivyo kwa makundi mengine ya rika. Wahusika ni watu au viumbe ambao watunzi huwabuni na kuwatumia katika kazi ya fasihi kuwakilisha tabia za watu katika maisha halisi (Mlacha & Madumulla, 1995). Wahusika ni miongoni mwa vipengele vya fani katika kazi ya fasihi, ukiwamo utanzu wa riwaya. Kipengele hiki ni muhimu katika kazi yoyote ya fasihi kwa sababu hutumiwa kama midomo na mabaragumu ya watunzi kufikisha fikra zao kwa hadhira.

Hata hivyo, uhusika wa kundi la vijalunga bado haujapewa nafasi ya kutosha katika uhakiki wa kifasihi na utafiti. Hata hicho kiasi kidogo ambacho kundi hili limepewa katika uhakiki na tafiti, mara nyingi, huchanganywa kwa kuitwa watoto au vijana. Kwa jumla, fasihi ya vijalunga huchanganywa katika fasihi ya watu wazima au fasihi ya watoto (Bakize, 2004). Hali hii ya kutofanyiwa kazi kwa kiasi cha kutosha inaweza kudumaza na kukwaza ufahamu wa jumla wa wanajamii kuhusu kundi-rika hili pamoja na uhusika wao katika bunilizi za kifasihi. Makala hii inashughulikia wahusika vijalunga waliotumiwa katika riwaya ya *Rosa Mistika*.

**Maelezo mafupi kuhusu riwaya ya *Rosa Mistika***

*Rosa Mistika* ni riwaya iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1971. Riwaya hii yenye mawanda ya kijamii ina sehemu kubwa mbili. Sehemu ya kwanza ina sura saba zinazoelezea mapito ya Rosa toka akiwa mtoto hadi anamaliza kidato cha nne. Sehemu ya pili ina sura tano zinazofafanua kuharibika kwa tabia ya Rosa pamoja na kilele cha anguko, yaani kifo chake. Fani ya riwaya ya *Rosa Mistika* ni nyepesi ikiwa na sifa za jumla za kuwa na usimulizi wa moja kwa moja, lugha nyepesi inayoeleweka kirahisi, pamoja na kutumia vitushi vyenye visababishi vilivyo bayana kwa msomaji (Ponera, 2014). Kwa jumla, hii ni riwaya nyepesi kueleweka ikilinganishwa na riwaya zake zilizofuatia, hasa *Nagona* na *Mzingile*. Riwaya hii ina ufumbaji ambao unaanzia toka kwenye jina lenyewe la riwaya, *Rosa Mistika*, lenye maana ya 'Waridi lenye Fumbo'. Kwa hiyo, ikiwa msomaji anaisoma kwa juujuu huenda asiibuke na kiwango cha kutosha cha uelewa. Sehemu kubwa ya mandhari inayosawiriwa katika riwaya hii ni ya Wilaya ya Ukerewe, na, kwa kiasi kidogo, imetumika miji ya Mwanza na Morogoro. Mtunzi

ameanza kwa kuyasawiri mandhari ya Kijiji cha Namagondo kilichomo katika Kisiwa cha Ukerewe. Vitushi vyote vya riwaya hii vimeshikizwa katika mihimili mikubwa miwili ambayo ni migogoro ya kimalezi na makuzi katika jamii, pamoja na nafasi ya miongozo ya kiteolojia katika jamii. Masuala haya yote yanamzonga mhusika mkuu ambaye ni Rosa.

Mwandishi ameanza kulitongoa fumbo lake kwa kumwelezea Rosa akiwa mtoto na kijalunga mwema sana. Kimalezi, tangu akiwa mtoto, Rosa alikuwa anabinywa na fikra na miongozo ya baba yake, Mzee Zakaria, ambaye hakuwa tayari kumwona Rosa akitumia uhuru wake kuchangamana na watoto wenzake. Zaidi, Mzee Zakaria hakuwahi kumpa mwanawe huyu mafundisho yoyote ya kukabiliana na vitimbi vya walimwengu pamoja na ulimwengu uliojaa mabadiliko. Mabadiliko ya msingi yaliyomkumba Rosa ni yale ya kibayolojia ambayo yanafikia kilele akiwa katika shule ya *Rosary*—hapa tayari alikuwa nje ya minyororo ya baba yake. Ni katika wakati huu, ndipo Rosa, kutokana na kukosa miongozo sahihi ya kimalezi kutoka kwa wazazi, pamoja na walimu wake, anajikuta akibadilika na kuwa malaya maarufu.

Riwaya hii ni fumbo la kijamii ambalo linapofumbuliwa na msomaji, mambo mengi yaliyosokotana yanaanikwa. Mathalani, wakati jicho la haraka na la jumla likijielekeza katika umalaya wa Rosa, jicho la ndani linatumulikia uasherati pia wa vilajunga wa kiume na hata walimu wenye jukumu kubwa la kuwalea vijalunga wawapo katika taasisi za elimu. Pia, kuna fumbo la safari ya maisha ya binadamu, kwamba si rahisi kuutabiri mwisho wa mwenendo au maisha ya binadamu hata kama ataonesha tabia za namna yoyote katika maisha yake ya awali. Halafu, kuna suala la kupwaya kwa dhima na mikakati ya asasi za dini na viongozi wake katika

kutibu vidonda vya kimaadili vilivyotapakaa kwa waumini wake. Mkorogano mzima wa malezi, makuzi, na maisha yote ya kijalunga Rosa unaishia kwa Rosa kujiua. Tukio hili la kujiua linasababisha afunguliwe kesi kwa Mungu. Kwa jumla, riwaya hii inaing'ong'a mifumo ya malezi ya vijalunga, hususani wa kike, wawapo katika ngazi mbalimbali, kuanzia ngazi ya familia hadi taasisi za kielimu na zile za kiroho.

## Kiunzi cha Nadharia

Maudhui ya makala hii yanatokana na utafiti ulioongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Waasisi wa nadharia hii ni George Wilhelm Hegel (1770 - 831), Friedrich Schiller (1759 -1805), na Gustave Flaubert (1821-1880). Wadau hawa wanapendekeza matumizi ya neno uhalisia katika kuelezea kazi za kifasihi ambazo zinawakilisha maisha ya kijamii ambayo yana wahusika wanaotenda mambo kulingana na hali mbalimbali zinazowazunguka. Nadharia hii husisitiza usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake (bila kupausha, kupindisha wala kudondosha jambo). Anyango (2016) anabainisha kuwa Nadharia ya Uhalisia ilianza kuhusishwa katika fasihi kwa sababu waasisi wa nadharia hii waliona kuna uhusiano mkubwa kati ya kazi za kisanaa na mtazamo wa msanii kuhusu jamii anamopatikana. Larkin (1977) anasisitiza kuwa, kulingana na mtazamo wa nadharia hii, msanii anafaa kuwa kurunzi ya jamii. Hii ni kwa sababu jukumu lake kubwa ni kuumulika ukweli wa maisha halisi ya jamii ili, kama kuna namna yoyote ya kupotoka, awarudishe watu katika unyoofu au ustawi.

Aidha, Wafula na Njogu (2007) wanabainisha kuwa istilahi ya uhalisia hufafanuliwa kwa kuhusishwa na mikondo mitatu—mwelekeo, mbinu ya kisanaa, na mbinu ya kihakiki. Uhalisia unapotazamwa kwa mkondo wa mwelekeo, huonwa kama seti ya taratibu au njia za kisayansi za kutekeleza

jambo. Kwa hiyo, taratibu au njia hizi hupinga mtazamo wa kinjozi juu ya maisha. Unapotazamwa kama mbinu ya kisanaa, uhalisia huhusishwa na mbinu yenye mashiko katika kusawiri hali halisi ya maisha ya watu kwa nje na kwa ndani (hali ya kisaikolojia ya watu). Unapotazamwa kama mbinu ya kihakiki, uhalisia huwa nyenzo ya kumulika jinsi mtunzi alivyozingatia ukweli na urahisi katika kusana vipengele vya kazi yake, hususani muundo na muwala. Hivyo, uhalisia huichambua kazi kwa kuzingatia hali halisi, huku ikimakinikia uhusika, lugha wanayotumia wahusika, na vipashio vya kihistoria vinavyosababisha mabadiliko makubwa ya kijamii.

Ifuatayo ni misingi ya Nadharia ya Uhalisia: Msingi wa kwanza unaitaka kazi ya fasihi kuwasilisha maudhui kwa kuzingatia ukweli, ukamilifu, uaminifu na usahihi mkubwa. Hii inamaanisha kuwa kazi ya fasihi isimulie mambo kama yanavyotokea katika jamii inayorejelewa kwa kuakisi maisha katika nyuga zote kama vile siasa, uchumi, na utamaduni. Msingi wa pili unasisitiza vipengele mbalimbali vya kazi ya fasihi kama vile mazingira, mandhari na wahusika kusawiriwa kikwelikweli ili kuyaakisi maisha ya kila siku (kwa kuzingatia furaha, huzuni, matumaini, matazamio, na matatizo). Msingi wa tatu unasisitiza kazi ya fasihi idokeze hali halisi ya kisaikolojia ya wahusika. Msingi wa nne unahusu kazi ya fasihi kuleta athari kwa hadhira, yaani kazi ya fasihi iwe kama malighafi ya kuleta mabadiliko katika jamii.

Msingi wa kwanza, wa pili, na wa tatu ilitumika katika utafiti na mjadala kuhusu namna riwaya ya *Rosa Mistika* inavyosawiri zila na changamoto za vijalunga. Msingi wa nne umetumika kama nyenzo au ithibati ya kuhitimishia namna riwaya ya *Rosa Mistika* inavyoweza kusimama kama kurunzi ya kuendesha mchakato wa kulea vijalunga.

## Methodolojia ya Utafiti

Data zilizozaa maudhui ya makala hii zilikusanywa kwa kutumia njia ya uchambuzi wa matini. Mwandishi wa makala hii alisoma na kuchambua riwaya teule ambayo ni *Rosa Mistika* (2000). Riwaya hii ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa, ambapo, kupitia usomaji wa awali, mwandishi alibaini kuwapo kwa uhusiano baina ya aina ya malezi waliyokuwa wanapewa vijalunga na changamoto walizokuwa wanakutana nazo. Euphrase Kezilahabi alianza kuitunga wakati akiwa mwanafunzi wa ngazi ya sekondari na kuikamilisha akiwa chuo kikuu. Hivyo, maoni yetu ni kuwa riwaya hii inaonekana kuwa kipitishio kizuri cha fikra zilizokuwa zinachemka kichwani mwa mtunzi katika zama za ujalunga wake. Data zilizolengwa zilikuwa za kitaamuli, yaani data zenye mwegamo wa kimaana. Data zilizopatikana zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Data hizo zilipangwa katika makundi mbalimbali ambayo yalipewa hadhi ya misimbo, ambapo kila msimbo uliwakilisha maana mahususi. Kisha, misimbo hiyo iliwianishwa, kuchujwa, na kupangwa ili kuibua ruwaza mpya ya maana inayokidhi lengo kuu la makala.

## Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti kuhusu namna gani riwaya ya *Rosa Mistika* inafaa kuwa kurunzi ya malezi ya vijalunga. Ilibainika kuwa riwaya hii inafaa kutumika kama kurunzi ya kuwalea vijalunga, hatimaye, kuwa na jamii yenye ustawi wa kimaadili. Sehemu hii imegawanyika katika vijisehemu vifuatavyo: zila za changamoto za vijalunga katika riwaya ya *Rosa Mistika* na changamoto za vijalunga katika riwaya ya *Rosa Mistika*.

### Zila za changamoto za vijalunga katika riwaya ya *Rosa Mistika*

Katika utangulizi, imeelezwa kuwa, katika muktadha wa kifasihi, dhana ya zila huchukuliwa kuwa ni msukumo ambao huwa chanzo cha hali au matokeo hasi kama vile anguko. Vilevile, katika ufafanuzi wa sifa bainifu za vijalunga, imeelezwa kuwa sehemu kubwa ya tabia zinazooneshwa na vijalunga huwa na mwelekeo hasi kulingana na maadili ya jamii. Hivyo, kijisehemu hiki kinaeleza hoja zinazowasukuma vijalunga kudhihirisha sifa na tabia hizo bainifu. Hoja zinazoelezwa ni tatu. Nazo ni mabadiliko ya mahitaji, wazazi au walezi kukosa elimu ya kuishi na vijalunga, pamoja na kupwaya kwa mikakati ya umma kuhusu maisha ya vijalunga. Hoja hizi zinaelezwa huku zikiegemezwa katika riwaya teule.

***Mabadiliko ya mahitaji ya vijalunga***

Wahusika vijalunga waliotumiwa katika riwaya ya *Rosa Mistika* wamesawiriwa wakikumbwa na mabadiliko kadhaa. Kwa mujibu wa McNeely (2003), umri wa ujalunga hutawaliwa na mabadiliko makubwa ya kimwili, kiakili, na kimatarajio. Kimwili, kijalunga hukabiliwa na mabadiliko kwenye vipengele vingi, kikiwamo kipengele cha hamu ya kufanya mapenzi, uwezo wa kutungisha mimba au kubeba mimba (kwa kijalunga wa kiume na wa kike, mtawalia). Mabadiliko haya yamearidhiwa vizuri kwa vijalunga waliomo kwenye riwaya ya *Rosa Mistika* kama vile Rosa, Charles, na Flora. Mathalani, mwandishi anatuonesha mabadiliko ya Flora kupitia nukuu ifuatayo:

> Flora akienda kuoga hujiangaliangalia kwa muda mrefu kabla ya kuoga. Hutazama matiti yake ambayo sasa yalikuwa yanaanza kuwa makubwa; hujipapasapapasa kwa mikono kutoka mgongoni mpaka pale matako yanapotelemkia; halafu huanzia kifuani mpaka pale tumbo linapotelemkia; halafu tena hujiangaliaangalia ... (uk. 4).

Uchunguzi huu wa Flora katika mwili wake unatumulikia kuwa amebaini kuwapo kwa mabadiliko. Aidha, unatumulikia hamu yake ya kutaka kujua mambo yanayoambatana na mabadiliko hayo. Wakati umbo la nje la nukuu hii linatuonesha namna Flora anavyochunguza mabadiliko anayoyaona katika mwili wake (kama vile mtutumko wa matiti na makalio), umbo lake la ndani linatuangazia msongano wa mawazo akilini mwa Flora kuhusu mabadiliko hayo. Hali hii ya msongano wa mawazo inayakinishwa na msingi wa tatu wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza kuwa kazi ya fasihi idokeze hali halisi ya kisaikolojia ya wahusika.

Kiakili, kijalunga pia hujikuta katika uwezo mkubwa zaidi wa kufikiri kuliko aliokuwa nao kabla ya kubalehe. Aghalabu, mabadiliko ya kibayolojia yanayotokea mwilini mwake huwa kichokoo muhimu cha kujidadisi yeye mwenyewe, vijalunga wenzake, na jamii kwa jumla. Mathalani, kwa vijalunga wa kiume, ujitokezaji wa ndoto nyevu katika siku za mwanzo huchochea maswali mengi akilini mwao (Garland, 2001). Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* anatuaridhia hali hii kupitia maswali ya kusaka uhuru kutoka kwa ama wazazi au walezi wa shuleni kwao ambayo Rosa na Flora wanajiuliza. Katika mfano mmojawapo wa harakati za kuusaka uhuru kutoka kwa baba yake, Mzee Zakaria, Rosa alidiriki kujibizana na mzazi wake huyo. Mwandishi anasawiri majibizano hayo yasiyo ya kimaadili kupitia tukio la Rosa kufuatwa nyumbani na kijana mwenye gari. Hapo ndipo Mzee Zakaria alianza kufoka:

> Rudi na motakaa yako! Unafikiri hapa kuna wasichana wengi wa kuchukua kwa gari. Toka hapa, masikio makubwa mithili ya punda! Na wewe Rosa usitoe pua yako nje! Nisikuone unatoka hapa! Unafikiri uko Morogoro! (uk. 58).

Anayetukanwa na kufukuzwa katika tukio hili ni mkuu wa wilaya aliyekwenda nyumbani kwa Zakaria kumfuata Rosa aliyerudi hapo kwa mapumziko akitokea chuo cha ualimu. Matusi haya ya Zakaria ni mwendelezo wa mfumo wake wa kuwalea watoto wake wa kike kwa kuwabana. Hata hivyo, anashindwa kung'amua kuwa Rosa huyu anayemkataza hapa ameshapea katika medani ya ngono. Matokeo yake, Rosa aliamua kutumia fursa hiyohiyo kulipiza uchungu mwingi aliofanyiwa na baba yake kwa kumwambia, "Kila wakati unatuchunga. Unafikiri utatuoa wewe!" (uk. 58). Ni wazi kijalunga huyu alikuwa amechoka kubanwa. Hivyo, alihitaji uhuru.

Chanzo cha mabadiliko ya kimatarajio, kwa mujibu wa Hazen (2008), ni jamii yenyewe, wakiwamo wazazi au walezi, ambao 'humlazimisha' kijalunga atende au aenende kwa kiwango cha juu cha ufanisi kinachoendana na kile wanachodhihirisha watu wazima kwa hoja kuwa 'sasa umekua'. Urudiaji wa hali hiyo ya 'kulazimisha' kumhamisha kijalunga kutoka hatua ya utoto kwenda utu uzima humfanya kijalunga naye aunde matarajio ya maisha kwa kiwango cha juu kuliko umri na uwezo wake. Mathalani, hoja ya kuambiwa kuwa 'sasa amekua' inaweza kumfanya aanze kuwaza kutenda kama watendavyo wakubwa wake. Hivyo, urushaji huo wa kiwango cha matarajio, hatimaye, huweza kumfanya kijalunga akafanya au akaenenda katika namna inayokiuka maadili ya jamii yake.

Mabadiliko haya yote husababisha kubadilika kwa aina, kiwango, na mwelekeo wa mahitaji ya kijalunga kijamii, kimwili, na kiakili. Mchakato wa kusaka namna ya kujitimizia au kuendana na mabadiliko hayo ya

mahitaji, hatimaye, huweza kumfanya kijalunga akaangukia katika tabia au mwenendo mbaya.

***Ukosefu wa elimu ya kuishi na vijalunga***

Zila nyingine kwa vijalunga kutumbukia katika tabia hasi ni wazazi au walezi kukosa elimu ya kuwamudu vijalunga. Vijalunga ni kundi moja tu kati makundi mbalimbali yanayostahili malezi maalumu. Makundi mengine ambayo si sehemu ya maudhui ya makala hii ni watoto na vijana. Mbinu za malezi ya vijalunga ni somo muhimu ambalo kila mzazi au mlezi anapaswa kulifahamu kwa sababu kila kundi lina mbinu zake za kulilea (Berlin, 2009). Isivyo bahati, wazazi au walezi wengi hawana maarifa na ujuzi wa kutofautisha malezi ya watoto, vijalunga, na vijana. Aghalabu, huwalea vijalunga au vijana kwa kutumia mbinu zilezile ambazo huzitumia kuwalea watoto. Miongoni mwa madhara yanayotokea katika hali hii, chambilecho Spano (2004), ni vijalunga kuona kama wanadharauliwa, hivyo, kuanzisha ukinzani. Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* anaisawiri vizuri zila hii kupitia Mzee Zakaria, baba yake Rosa, ambaye aliamini kuwa silaha pekee ya kuwalea vijalunga wake wa kike ni kuwa mkali na kuwabana. Mfano mmojawapo ni pale tunapomsikia mzazi huyo akisema: "… Nisikuone unatoka hapa! Unafikiri uko Morogoro!" (uk. 58). Kupitia msingi wa kwanza wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza kuwa kazi ya sanaa isawiri mambo kikwelikweli (bila kupindisha wala kupausha), nukuu hii inatuthibitishia kuwa Euphrase Kezilahabi ameyavaa vyema matukio yanayotokea katika jamii. Hii ni kwa sababu, anayemfukuza kijalunga katika nukuu hii ni baba kama ambavyo hutokea katika maisha yetu. Katika hali halisi, ni vigumu kwa mama kumfukuza mwanawe kutoka nyumbani hata awe amefanya kosa kubwa.

Pia, mwandishi anaonesha upofu wa jamii nzima katika kuishi na vijalunga. Mathalani, anatuonesha jinsi watu wazima wasivyojali kufanya matendo yanayokiuka maadili mbele ya watoto au vijalunga. Katika tukio mojawapo la jinsi hii, mwandishi anatuambia:

> Ilikuwa mara ya kwanza kwa Stella kuona walevi—matendo na maneno yao. Honorata alikuwa akiosha bakuli, Stella alipomwambia: "Honorata! Angalia, aa! Aa! Aa! Honorata akatoa macho mara moja tu: Mtu mmoja alikuwa anakojoa karibu yao. Stella mwishowe aliwazoea, kwani aliwaona wakikojolea michungwa, migomba, maua yao hata nyumba (uk. 19).

Tukio linalobainishwa katika dondoo hili lilitokea nyumbani kwa Mzee Zakaria wakati mkewe, Regina, alipopika pombe ya kuuza ili apate fedha za kumsomeshea Rosa. Huyu aliyekuwa anakojoa ni mmoja wa wateja waliokuja kununua na kuinywa hapohapo nyumbani kwa Mzee Zakaria. Alifuatiwa na wenzake wengi ambao walikojolea mimea iliyozunguka nyumba hiyo. Tukio hili pia linaafikiana na Nadharia ya Uhalisia kupitia msingi unaosisitiza kuwa kazi ya sanaa inatakiwa kusawiri mambo kama yanavyotokea katika jamii. Mtu anapotopewa na ulevi, utashi wake hupungua; hivyo, huweza kufanya jambo lolote bila aibu. Matendo kama haya yanapofanywa mbele ya watoto na vijalunga husababisha wayaone kama ya kawaida, hatimaye, kuwachochea kuingia katika maadili mabaya. Kwa upande mwingine, yanawapunguzia wazazi au walezi nguvu na uhalali wa kuwaonya na kuwarekebisha watoto na vijalunga.

***Kupwaya kwa mikakati ya kijamii kuhusu vijalunga***

Dhana ya 'mikakati ya kijamii' tunaitumia katika makala hii kumaanisha mipango, sera, programu, sheria, au kanuni zinazoandaliwa na jamii mahususi kwa ajili ya vijalunga. Mathalani, jamii inatakiwa iwe na urazini

katika kuandaa na kuchagiza sanaa na michezo ya vijalunga. Hali halisi kuhusu mifano ya maeneo haya mawili—ya michezo na sanaa—si ya kuridhisha kwa vijalunga. Hali iko hivyo pia katika nyuga nyingine nyingi zinazohusiana na maisha ya vijalunga. Kiwango cha utambuzi wa kundi la vijalunga si cha kuridhisha kwani sehemu kubwa ya jamii huwatambua watu walio katika umri wa ujalunga kama vijana. Tumekwishaeleza katika sehemu zilizopita kuwa haya ni makundi tofauti. Hivyo, hadhi na mahitaji yake pia ni tofauti. Namna hiyo ya kutowatambua inasababisha kupwaya kwa mikakati ya kijamii kuhusu ustawi wa vijalunga.

Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* anawasawiri vijalunga wakiendeshwa na utashi wa wazazi au walezi pamoja na fikra zao. Mwandishi haoneshi kama kuna juhudi za kuridhisha za kijamii katika kushughulikia masuala yanayowahusu vijalunga. Mathalani, kwa kutumia maudhui yaliyofungwa kwenye tamathali, mwandishi anatuonesha kuwa jamii haipatilizi matatizo ya kijalunga Rosa. Zaidi, hata pale wanajamii wachache wanapojielekeza kushughulikia matatizo ya kijalunga huyu, bado hawapatii. Kuhusu sababu ya kutopatia huko, mwandishi anasema: "… moto ulikuwa ukiwaka upande wa Kusini lakini wao walikuwa wakizimisha upande wa Kaskazini (uk. 33). Kwa jumla, hali hii ya kukosekana au kupwaya kwa mikakati mahususi inayowalenga vijalunga inasababisha masuala mengi yanayohusiana na vijalunga yachanganywe na ama watoto au vijana. Hali hiyo inaleta mtanziko wa kifikra na kimwenendo kwa vijalunga.

### Changamoto za vijalunga katika riwaya ya *Rosa Mistika*

Hoja zilizowasilishwa katika kijisehemu kilichopita kuhusu zila mbalimbali zinatoa dira ya kuwapo kwa changamoto ambazo vijalunga hukumbana

nazo katika maisha yao. Changamoto zinazojadiliwa ni kukosa haki ya malezi, kupata mimba wakiwa masomoni, kuambukizwa magonjwa, na kutengwa.

***Kukosa haki ya malezi bora***

Imekwishaelezwa katika sehemu mbalimbali za makala hii kuwa umri wa ujalunga hutawaliwa na mabadiliko makubwa ya kimwili, kiakili, na kimatarajio. Mabadiliko haya huhitaji kuongozwa na kudhibitiwa na malezi sahihi. Malezi ni miongoni mwa haki za kijalunga. Wahusika vijalunga waliosawiriwa katika riwaya ya *Rosa Mistika* wanaonekana kuikosa haki hiyo ya malezi. Haki mojawapo ya malezi wanayoikosa vijalunga hao ni uhuru. Binadamu huhitaji uhuru katika kuishi kwao ili kuweza kuyafahamu mazingira yao na kuyamudu. Kwa upande wao, vijalunga huwa na mahitaji makubwa ya uhuru kutokana na mabadiliko tuliyokwishayadokeza.

Euphrase Kezilahabi anaeleza kuwa kitendo cha vijalunga kubanwa kibubusa—kwa kutumia ukali bila maelekezo—husababisha washindwe kufahamu mambo mengi, hususani ya mahusiano ya kingono, hatimaye, kushindwa kukabiliana nayo. Anaielezea dhana hiyo ya uhuru wa vijalunga kwa kutumia maelezo yafuatayo ya kitamathali:

> Maisha ya binadamu ni kama miti. Mti unahitaji maji, hewa na mwanga. Kama mti ukinyimwa mwanga wa kutosha na miti mingine, utaukuta unajaribu kupita miti yote ili upate mwanga (uk. 47).

Nukuu hii inawakumbusha wazazi na walezi wa vijalunga kuwianisha vipengele vya malezi kama vile elimu (mafunzo na maelekezo), ufuatiliaji, udhibiti, na ukali wa kadiri. Miongoni mwa madhara yatakayotokea kwa vijalunga ikiwa utakosekana uwiano katika vipengele hivyo, hususani

kwenye suala la mahusiano, ni vijalunga kutumbukia kwenye ngono kiupofu. Akiisawiri hali hiyo, mwandishi wa riwaya hii anasema:

> Wanachukuliwa na wapishi wa Wahindi mjini … Kwa sababu ya kulindwa, wanakuwa kama wanyama. Wanapenda mtu yeyote yule apataye bahati kuonana nao. Wanapoteza uwezo wao wa kuchagua (uk. 43).

Katika nukuu hii, mwandishi anaeleza athari za kukosa kuyafahamu mazingira na kukosa tajiriba ya kufanya uchaguzi sahihi katika maisha. Hapa, mwandishi anawaonesha wasichana wa shule wakikosa uwezo wa kujua sifa za mwanamume anayefaa na asiyefaa kuwa na uhusiano naye wa kimapenzi na/au ndoa.

Hoja muhimu inayopaswa kufahamika na wazazi na walezi ni kuwa vijalunga wanahitaji uhuru unaoendana na maelekezo. Maelekezo hayo, yumkini, huendana na mzazi au mlezi kumfahamu vilivyo kijalunga wake, yaani kufahamu uwezo wake wa kiakili, mambo anayoyapendelea, marafiki wanaomzunguka, na hatari zinazomzunguka. Mzazi anayesawiriwa katika riwaya hii alikuwa na ufahamu wa mambo haya? Alikuwa anatumia mbinu zipi za malezi ya wanawe, wakiwamo vijalunga? Euphrase Kezilahabi anajibu maswali haya kupitia nukuu zifuatazo:

> Alijidai kwamba yeye alifahamu jinsi ya kulea binti zake—hasa alipokuwa amekunywa kidogo. Hakufahamu kwamba Rosa alikuwa katika rika baya; na kwamba, ukali ulikuwa haufai. Hakufahamu kwamba mabinti wanahitaji uhuru fulani kutoka kwa baba zao; hakufahamu kwamba Rosa alihitaji kuwafahamu wavulana (uk. 9).

Hapa, mwandishi anamng’ong’a Mzee Zakaria kwa kutojua malezi ya vijalunga waliokuwa katika familia yake. Pamoja na ujinga huo, bado mzazi huyu anajitapa kuwa anafahamu jinsi ya kuwalea wanawe.

Kuhusu mbinu alizokuwa anatumia Mzee Zakaria kuwalea wanawe, katika riwaya hii, tunaoneshwa kuwa kiongozi huyu wa kaya alikuwa anatumia ukali, vipigo, na vifungo. Mathalani, katika ukurasa wa 6 - 7, mwandishi anaonesha namna Rosa anavyopigwa na baba yake hadi kutoka damu puani na mdomoni. Kipigo hiki kilitokana na kufumwa na barua na fedha kutoka kwa Charles. Euphrase Kezilahabi analisawiri tukio hilo kwa kueleza hivi:

> "Lete hiyo barua, iko wapi? Pamoja na shilingi ulizopewa. Unafikiri sisi hapa maskini!" Rosa alipigwa tena na tena, makofi yalikwenda mfululizo hata damu ikamtoka puani na mdomoni.
> Alilia, "Baba nihurumie, sitarudia tena, nimekoma."
> Rosa alinyang'anywa shuka, chupi ilimuokoa lakini matiti yalikuwa nje. Ole wao watakaoyaona matiti ya binti zao!

Nukuu hii inaonesha jinsi Mzee Zakaria alivyokuwa na malezi yaliyoegemea kwenye mbinu ya kipigo. Mwandishi anamalizia nukuu hiyo kwa ubeuzi mkali kupitia kidole cha ole anachomwonesha Mzee Zakaria baada ya kuyaona matiti ya bintiye wakati anamwadhibu. Mbinu hizo za malezi ziliendelea kama mwandishi anavyosisitiza:

> Hivyo ndivyo Rosa alivyolelewa; hivyo ndiyo alivyotunzwa; hivyo ndivyo alivyochungwa na babake. Tangu siku hiyo alikoma kutembea na mvulana yeyote. Na Zakaria alipojua hayo alifurahi sana. Alijidai kwamba yeye alifahamu jinsi ya kulea binti zake, hasa alipokuwa amekunywa kidogo (uk. 9).

Hivyo ndivyo Rosa na nduguze walivyokuwa wakilelewa na baba yao, Mzee Zakaria. Hali hii ilichangia sana kuyaharibu maisha yao, hususani Rosa na Flora. Mbinu hiyo ya Mzee Zakaria kuwalea vijalunga wake kwa njia ya kuwapiga iliwajengea woga. Pia, iliwanyima fursa vijalunga hao kuwafahamu wanadamu wengine, hususani walio na jinsi tofauti na wao, kutokana na kutochangamana nao.

Euphrase Kezilahabi anaifundisha hadhira kuwa mabadiliko yanayowapata vijalunga ni ya asili. Hivyo, hayawezi kuzuilika, bali yanatakiwa kuongozwa. Kwa namna ya kifutuhi, mwandishi huyu anatuonesha kuwa ukali na udhibiti wa kifungo aliokuwa anauonesha Mzee Zakaria kwa vijalunga wake haukuweza kukomesha ashiki ya kufanya mapenzi katika akili na mwili wa Rosa. Jambo hili limesawiriwa kupitia ndoto ifuatayo:

> Baada ya muda usingizi ulimchukua. Alimwona baba yake akitembea barabarani na mbwa. Mbwa huyo alikuwa amefungwa kamba shingoni. Mbwa aliona mbuzi. Alikata kamba na kukimbia. Alimrarua mbuzi vipande vipande .... Rosa aliamka, alilala, na usingizi ulimchukua tena. Aliona kijana mwembamba mwenye ndevu nyingi akimtazama kwa macho yenye huruma. Rosa alipomwona alimkimbilia na kumkumbatia akisema kwa sauti, lazima unioe, ukinikataa wewe maisha yangu yamekwisha .... (uk. 32).

Ndoto zote hizi zinahusiana na kani ya asili inayoamsha ashiki ya mapenzi. Msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza kuwa matini ya kifasihi lazima ihusiane na yanayojiri katika jamii unatuongoza kufahamu kuwa mbwa aliyefungwa kamba shingoni kwenye ndoto hii ni yeye Rosa anayechungwa na kufungiwa ndani na Mzee Zakaria, na mbuzi aliyeonwa ni mwanaume. Kutokana na kuzidiwa na hamu ya kutaka kufanya mapenzi, Rosa alijichoropoa kutoka katika kifungo cha baba yake na kuwakimbilia wanaume ili wakate hamu yake.

Katika kudhihirisha kuwa amemudu kuwasawiri wahusika wake katika maumbo ya nje na ya ndani kama inavyosisitizwa na Nadharia ya Uhalisia kupitia msingi unaotaka kazi ya fasihi idokeze hali halisi ya kisaikolojia ya wahusika, mwandishi anamsawiri Rosa akiota ndoto ya pili. Kabla ya kuieleza ndoto hii ya pili, ni vyema hapa tufafanue kuwa ndoto anayoota mwanadamu hutokana na akili yake kuakisi yale yanayomtokea katika

maisha yake ya kila siku. Ball (2003) anaongezea kuwa ndoto ni namna ya akili kujisafisha dhidi ya mawazo mbalimbali (hasa magumu) ambayo humzonga mwanadamu na kujielekeza kwenye ridhiko la nafsi. Ndoto hiyo ya pili haijatumia lugha ya picha, iko bayana. Mwandishi anaeleza:

> Thereza alikuwa bado hajaelewa Rosa alipomrukia na kumkumbatia. Waliangushana kitandani. Rosa alianza kumbusu, lakini tamaa yake haikuweza kupungua. Rosa alihitaji ule mkwaruzokwaruzo wa aina ya pekee. Mkwaruzokwaruzo wa ndevu na manyoya ya tumboni. Zaidi ya hayo, moto ulikuwa ukiwaka upande wa Kusini lakini wao walikuwa wakizimisha upande wa Kaskazini (uk. 33).

Ndoto hizi mbili zina kiwango kikubwa cha ushikamani. Hii ni kwa sababu ndoto ya pili inaungana au kuiendeleza ndoto ya kwanza. Ndoto zote hizi zinasisitiza kuwa mabadiliko ya kupata hamu ya kufanya mapenzi ni ya asili. Mwandishi anabainisha kuwa cheche za mapenzi zilizowashwa na ndoto ya mwanzo zilikuwa kubwa kiasi cha kumsukuma Rosa kufanya jaribio la usagaji—kumbaka mwanafunzi mwenzake aliyelala katika chumba hicho. Kutaka kufanya mapenzi na kijalunga mwenzake wa kike ni hatua ya juu kabisa ya kuzidiwa na hamu. Tukio hili ni chanzo cha kutetereka kwa tabia ya Rosa. Ni wazi kuwa Rosa hakupewa elimu ya kukabiliana na mabadiliko ya mwili wake. Mwandishi anaibeua jamii kwa mbinu zake mbaya za kuwalea vijalunga kupitia sentensi, "… moto ulikuwa ukiwaka upande wa Kusini, lakini wao walikuwa wakizimisha upande wa Kaskazini".

Maoni yetu yanayotiliwa nguvu na msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaosisitiza kuwa kazi ya fasihi iwasilishe maudhui kwa kuzingatia ukweli, ukamilifu, uaminifu na usahihi mkubwa ni kuwa mwandishi ametumia dhana za 'Kaskazini' na 'Kusini' kwa usahihi kutokana na shabaha

anayoikusudia. Tunaamini kuwa dhana ya 'Kaskazini' imetumika katika muktadha huu kumaanisha mabadiliko ya akili, tabia na mwenendo, ilhali dhana ya 'Kusini' imetumika kumaanisha mabadiliko ya kibayolojia, yakiwamo masuala ya kani ya asili inayoleta hamu ya kufanya mapenzi pamoja na afya ya uzazi. Hivyo, ubeuzi huu unaikumbusha jamii kutumia mbinu sahihi za malezi zinazoakisi nyuga zote za mabadiliko ya vijalunga.

***Kupata mimba wakiwa masomoni***

Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Mistika* anawasawiri wahusika vijalunga wawili, Rosa na Flora, wakipata mimba wakiwa shuleni. Tunaoneshwa Flora aliyekuwa shuleni akimwandikia barua dada yake, Rosa, na kumweleza jinsi alivyotoa mimba akiwa katika 'Shule ya Jela' kama wanafunzi wenyewe walivyokuwa wanaiita shule yao ya sekondari. Kupitia maneno ya Flora katika barua yake kwa dada yake kuwa, "Mimba tu haiwezi kunifanya nikajiharibia maisha yangu kwa kuacha shule" (uk. 46), mwandishi anaonesha kuwa utoaji wa mimba haukuwa jambo zito katika akili ya kijalunga huyu. Akielezea zaidi kuhusu wanavyopata mimba wakiwa shuleni, Flora anasema:

> Tunalindwa kama watoto wadogo. Wanafikiri hata wakati wa livu watatuchunga! Wasichana wengi hapa wamekwishapata mimba na kufukuzwa wakati wakiwa hapa hapa shuleni (uk. 62).

Nukuu hii inatumulikia jambo muhimu kwa vijalunga wanaosoma. Vijalunga hawa wana sehemu mbili za kulelewa, nyumbani na shuleni. Hivyo, nukuu inabainisha kuwa hakuna urari wa kimalezi kwa kijalunga awapo nyumbani na shuleni. Kwa mara nyingine, Euphrase Kezilahabi anaonesha kuyafahamu vilivyo matukio yanayotokea katika jamii yake, hivyo, kuyasawiri katika riwaya hii kama inavyosisitiza Nadharia ya Uhalisia kupitia msingi unaosisitiza kazi ya sanaa kuiakisi jamii. Tatizo la

wanafunzi kupata mimba wakiwa masomoni ambalo mwandishi analisawiri katika riwaya hii lipo katika jamii zetu. Mathalani, kwa mujibu wa Sinkonde (2024), wanafunzi 194 walipata mimba ndani ya mwezi mmoja katika Wilaya ya Momba yenye shule za msingi 103 na shule za sekondari 13.

***Kuambukizwa magonjwa***

Mtunzi wa riwaya ya *Rosa Mistika* anaonesha kuwa baadhi ya vijalunga hupata magonjwa ya zinaa. Hili linabainika pale Flora anapomsimulia Rosa jinsi alivyoambukizwa magonjwa na mpenzi wake wakati akiwa shuleni Mwanza. Anaeleza, "Wanaume wengine wanadanganya. Kijana mmoja amekwishaniambukiza magonjwa. Lakini nimekwishahakikisha kuwa John hana magonjwa!" (uk. 63).

Miongoni mwa mafunzo ya nukuu hii ni kuwa vijalunga wengi hawashughulishwi na kupima afya zao kabla ya kujiingiza katika mapenzi. Matokeo yake, baadhi yao hujikuta wanaambukizana magonjwa.

Mfano mwingine wa vijalunga kuambukizwa magonjwa umo katika tukio la Rosa kung'ong'wa na wanafunzi wenziwe. Mwandishi anaandika, Rosa alikuwa hajitambui mpaka alipopitia kundi la wasichana. Alisikia moja wao akisema; "Maskini! Maskini hajitambui!" Rosa alijiangangalia nyuma alikuta nguo yake imeingia matakoni (uk. 55)".

Tukio hili linatuaridhia kijalunga Rosa akiwa amevaa nguo iliyogandia na kuingia kwa ndani katika maeneo yake ya siri. Licha ya tukio hili kusimuliwa katika hali inayoonekana kukiuka maadili ya jamii, hususani kupitia matumizi ya lugha isiyo na tasifida, maudhui na muktadha unaosawiriwa unaakisi maudhui ya Nadharia ya Uhalisia. Uakisi huo

unadhihirika kupitia msingi unaosisitiza kuwa vipengele mbalimbali vya kazi ya fasihi kama vile mazingira, mandhari na wahusika visawiriwe kikwelikweli ili kuakisi uhalisi wa maisha ya kila siku (ambayo yana furaha, huzuni, makosa, matatizo, na matumaini). Rosa, kama mwanadamu mwingine yeyote, anasawiriwa katika tukio hilo akiwa kwenye tatizo kubwa la ugonjwa ambao unamletea idhilali mbele ya vijalunga wenziwe.

Hali hii inayomkuta Rosa katika tukio hilo huwatokea pia vijalunga wengine katika jamii yetu. Kwa jumla, vijalunga wengi hujikuta wakiangukia katika tatizo la kuambukizwa magonjwa kutokana na kukosa elimu na maelekezo ya jinsi ya kudhibiti mabadiliko katika miili yao.

***Kutengwa na jamii***

Usawiri wa wahusika vijalunga katika riwaya ya *Rosa Mistika* umeibua changamoto ya vijalunga kutengwa na jamii inayowazunguka. Mwandishi anaonesha namna Rosa alivyotengwa na kuchukiwa na wanafunzi wenzake wakati akiwa Morogoro TC. Anasema, “Wanafunzi walianza kumchukia … Siku moja alipopita katika kikundi cha wavulana pale shuleni, alisikia mmoja akitema mate chini. “Amekwisha kazi huyu! Amekwisha kazi!” (uk. 55).

Hapa, tunaona namna Rosa anavyotengwa na wanafunzi wenzake kutokana na matendo yake. Mbali na kutengwa na wanafunzi wenzake, kijalunga huyohuyo (Rosa) anasawiriwa akitengwa na mzazi wake, Mzee Zakaria, kutokana na mabadiliko ya tabia. Kalamu ya mwandishi inatuthibitishia kutengwa huko kupitia maneno yafuatayo ya Mzee Zakaria: “Zakaria alianza kuguna tu na kusema, “Rosa ndiye nani?  Malaya hajawa mgeni wangu wala mtoto wangu” (uk. 57). Kwa jumla, mwandishi amekusudia

kuionesha jamii jinsi baadhi ya vijalunga wanavyotengwa na wanajamii waliomzunguka baada ya kukumbwa na changamoto.

Kutengwa huko kulimsumbua sana Rosa moyoni. Kulimpa mawazo mengi na kumnyima furaha, kwani baada ya kuchukiwa na watu wengine, alihitaji kufarijiwa na wazazi wake. Wakati akiwa anaitaraji faraja hiyo, baba yake, Mzee Zakaria, anafunua zaidi kinywa na kumkana, tena mbele ya kadamnasi, kwa kusema, “Rosa, tangu leo wewe si mtoto wangu” (uk. 58). Maneno haya makali na yenye kutamausha kutoka kinywani mwa baba yake yalimfanya Rosa ashindwe kujizuia. Naye alimjibu Mzee Zakaria kwa maneno makali kuwa, “… na wewe kuanzia leo siyo baba yangu” (uk. 58). Majibizano haya yanashadidia muumano wa maudhui ya riwaya hii na Nadharia ya Uhalisia. Hii ni kwa sababu misigano ya namna hii baina ya vijalunga na wazazi au walezi inadhihirika katika jamii. Aghalabu, vijalunga wanapokutwa na maanguko kama vile kupata ujauzito na kufukuzwa shule huishia kusemwa, kung’ong’wa, kufukuzwa au kutengwa na wazazi au walezi. Katika hali kama hii, vijalunga nao huchukua hatua ya kujihami kwa maneno au vitendo.

**Hitimisho**

Makala hii imebainisha kuwa vijalunga ni kundi-rika linaloishi katika jamii yetu likiwa limenasa katika zila zinazozaa changamoto nyingi katika maisha yao. Zila zilizojadiliwa katika makala hii ni tatu. Nazo ni mabadiliko ya mahitaji, wazazi au walezi kukosa elimu ya kuishi na vijalunga, pamoja na kupwaya kwa mikakati ya umma kuhusu maisha ya vijalunga. Makala imebainisha kuwa zila hizo huzaa changamoto ambazo ni kukosa haki ya malezi, kupata mimba wakiwa masomoni, kuambukizwa magonjwa, na

kutengwa. Kutokana na zila na changamoto zilizobainishwa, mikakati ifuatayo inapendekezwa ili kujenga ustawi wa vijalunga.

Mkakati wa kwanza ni wazazi na walezi wenyewe kupatiwa elimu ya kuishi na vijalunga. Elimu hiyo inaweza kutolewa kupitia vyombo vya habari kama vile magazeti, redio, na televisheni. Vilevile, inaweza kutolewa kupitia matangazo na/au vikao vinavyoratibiwa na ngazi za serikali za mitaa. Miongoni mwa maudhui ya elimu hiyo ni utambuzi wa maadili kwa wazazi au walezi, yaani wao wenyewe wanapaswa kufahamu jinsi mienendo yao inavyoweza kuwa na athari chanya au hasi kwa wanaowalea. Ufahamu huo utaenda sambamba na kujifunza mbinu za kuyalea makundi hayo. Mbinu hizo zinajumuisha kuwa nao karibu/kujenga nao urafiki, kufuatilia mienendo yao, pamoja na kufahamu maneno mazuri ya kuyatumia wakati wa kuwarekebisha au kuwaonya. Mathalani, tunaamini kuwa, kama Mzee Zakaria angefahamu vizuri kuwa Rosa na Flora walihitaji malezi tofauti na yale waliyokuwa wanapata watoto wake wadogo, Stella na Emmanuel, bila shaka, angewasaidia vijalunga wake kuepuka matatizo waliyopitia.

Mkakati wa pili ni kuimarisha utoaji wa elimu kuhusu mabadiliko ya mahitaji ya vijalunga. Jamii inapaswa kufahamu sifa na tabia za vijalunga ili iweze kutambua tofauti za mahitaji ya kila rika. Kufanya hivi kutasaidia kutekeleza hatua na mahitaji sahihi ya kimalezi kwa rika husika.

Mkakati wa tatu ni kuimarishwa kwa mikakati ya umma kuhusu maisha ya vijalunga. Jamii inatakiwa iwe na sheria, sera, na mipango madhubuti na inayotekelezeka kuhusu vijalunga. Sheria, sera, na mipango hiyo inatakiwa kugusa nyuga mbalimbali za maisha ya kijalunga kama vile michezo, haki,

elimu, na afya. Tunaamini kuwa kuwapo kwa sheria, sera, na mipango hiyo kutamfanya kijalunga awe salama na mwenye ustawi popote atakapokuwa—nyumbani au shuleni/chuoni.

Msingi wa nne wa Nadharia ya Uhalisia unaitaka kazi ya fasihi kuleta athari kwa hadhira, yaani kazi ya fasihi iwe kama malighafi ya kuleta mabadiliko katika jamii. Hoja mbalimbali zilizojadiliwa katika makala hii zimedhihirisha kuwa, ikiwa riwaya ya *Rosa Mistika* itasomwa na kufundishwa kwa umakini, ina uwezo mkubwa wa kuathiri mfumo wa malezi ya vijalunga, hatimaye, kuwaepusha na changamoto mbalimbali. Hivyo, riwaya hii inafaa kuwa kurunzi ya malezi ya vijalunga, hususani katika wakati huu ambapo dunia inapita katika mojawapo ya vipindi vyenye wingu zito la upogo wa kimaadili.

**Marejeleo**

Anyango, A.P. (2016). *Usawiri wa Uovu katika Riwaya Teule za Ben R. Mtobwa* (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Arnnet, D. (1999). *Developing Adolescent*. New York: American Psychologal Association.

Bakize, L.H. (2004). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Ball, P. (2003). *Interpret Your Dreams: Unlock Your Subconsciuos Mind*. London: Arcturus Publishing Ltd.

Berlin, L.J. (2009). *Research on Adolescent Development, Competence and Character*. Durham: University of Duke.

Degner, A.J. (2007). *The Definition of Adolescence*. New York: Ballantine Books.

Garland, A. (2001). *Frame Work for Action on Adolescents and Youth*. London: Penguine.

Hazen, T.M. (2008). *Self - Concept among Vulnerable Children na Adolescent: An Age of Storm and Stress*. New York: Cambridge University Press.

Kaplan, P.S. (2004). *Adolescence.* Boston: Houghton Mifflin Company.

Kezilahabi, E. (2005). *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Larkin, P. (1977). *Beyond Realism and Postmodernism*. Oxford: St. John's College University of Oxford.

McNeely, C. (2003). *Devision of General Pediatrics and Adolescent health*. Washington: University of Minnesota.

Mlacha, S.A.K. & Madumulla, J.S. (1995). *Historia na Maendeleo ya Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*: *Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu.* Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.

Ponera, A.S. (2014). *Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi* (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTU.

Shima, G.E. (2021). *Uwasilishaji wa Hisia za Watoto Kupitia Maigizo ya Utotoni* (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Sinkonde, D. (2024). Wanafunzi 194 Momba Wapewa Mimba Ndani ya Mwezi Mmoja. *Mwananchi*. Tarehe 16/5/2024 (uk. 1).

Spano, S. (2004). "Stages of Adolescent Development: Research Facts snd Findings". Inapatikana katika https://www.scribd.com/doc/315892300/stages-of-adolescent-development-philo-guys-docx. Ilisomwa tarehe 13/12/2023.

TET (2019). *Kiswahili Shule za Sekondari: Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita*. Dar es Salaam: TET.

TUKI (2006). *English - Swahili Dictionary 3rd Edition (Kamusi ya Kiingereza - Kiswahili Toleo la Tatu)*. Dar es Salaam: TUKI.

Wafula, R.M. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.